**Kila mtu ana malaika (2) - Mabalehe wanakabiliwa na hatari kubwa**
Mwandishi: Romie Singh - Mhariri: Saumu Mwasimba

**Wahusika:**

Daktari wa kiume (38)
Anita
Angela
Tom
Djamila
Annie
Jet
Ma Tilly

## Utangulizi

Karibu kwa mara nyingine katika kipindi cha sikiliza ujifunze ambapo tunaingia sehemu ya pili ya mfululizo wetu wa mchezo wa kuigiza Malaika wa kila.Ni ktu gani kinachowatumbukiza vijana katika hatari ya kimaisha?Je ni kwa sababu wanashawishika kiharihsi na makundi ya vijana wenzao,kwasababu wanatafuta mapenzi na kutambulika kwenye maisha ya uhusiano wa kimapenzi?

Angela alijimwaga kwenye sherehe na kupata ujauzito baada ya kulala na kijana asiyemjua na tena bila ya kutumia kinga ya mpira wa Kondom.Mamake ametishia kumfukuza nyumbani.Annie nae anaingia mtegoni.Ni msichana mwenye umri wa miaka 16 tu lakini mamake hajali anakokwenda mwanawe na wala nani anayekutana nae na tayari ana wavulana chungunzima ambao ni wa umri wake halikadhalika mwanamme mwenye umri mkubwa kumshinda yeye mwenyewe na huyu ndie baba sukari wake.

Ungana nasi basi ili upate kujua nini kitatokea katika sehemu hii ya pili ya mchezo malaika wa kila mtu.

## SURA YA KWANZA: Kwenye Kliniki.

| | |
|---|---|
| SFX: | Saumu ´za kuashiria ni hospitali |
| Daktari: | Naam sasa unaweza kuingia |
| SFX: | Mlango unafungwa,ndani ya ofisi simu zinalia. |
| Daktari: | Naam mimi ni daktari Majoro. Na kama ilivyoandikwa katika faili yako unaitwa Angela na umri wako ni miaka 17. Hmmmmm: kwa hivyo unafikiri umekomaa kiasi cha kutosha kulala lala na vijana? |
| Angela: | Daktari sio hivyo… nili… |

**Kila mtu ana malaika (2) - Mabalehe wanakabiliwa na hatari kubwa**
Mwandishi: Romie Singh - Mhariri: Saumu Mwasimba

| | |
|---|---|
| Anita: | Bwana Daktari hata mimi sikufahamu haya yote nimeshtuka kama wewe! |
| Daktari: | Wasichana wa siku hizi! Sasa hebu tuambie unasemaje?je unajutia vitendo vyako? |
| Angela: | Ndio Daktari. |
| Daktari: | Sawasawa, hebu tukuangalie… (anagusagusa tumbo la Angela) Hmmmm. Namsikia mtoto, lazima ujauzito huu uwe ni wa miezi sita hivi… Hata hivyo, tusubiri matokeo ya uchunguzi wa mkojo. Ntakuita baada ya dakika 10, tafadhali subiri hapo nje. |
| SFX: | Muziki wa kufunga |
| SFX: | Daktari akiitwa, Sauti ya mtoto akilia, mlango unafunguka |
| Daktari: | Sawa sawa Angela; njoo ndani tafadhali. |
| Anita: | Asante. |
| Daktari: | (akikatiza) Aah samahani bibi Selebi. Kuna masuala mengine ambayo ni ya mtu binafsi ambayo ninahitaji kuyajadili na mwanano peke yake. |
| SFX: | Mlango unafungwa sauti za simu chini kwa chini zinasikika. |
| Daktari: | Angela wewe sasa ni msichana mkubwa umepita umri wa miaka 16 na una haki ya kuweka mambo yako binafsi. |
| Angela: | Naam lakini mama pia anajua hata hivyo kuwa nina mimba ama sivyo? |
| Daktari: | Ndio, kweli u mjamzito, lakini kwa nini ukanyamaza kwa muda mrefu kiasi hiki? Hukufahamu kwamba umepata ujauzito? |
| Angela: | Ahh daktari nilikuwa najihisi tofauti kidogo lakini… |
| Daktari: | Matiti kwa mfano shemu nyingine lazima haya yote utambue kwamba sasa utakuwa ni mama! |
| Angela: | Sikuruhusiwa kuzungumzia uchafu huo nyumbani daktari. |
| Daktari: | Ni mwili wako tunaouzungumzia umesikia Angela! Sio uchafu kama unavyouita. Ok sasa kitu kimoja unapaswa kutambua, una haki ya kuamua kupima virusi vya HIV. Je unafahamu virusi hivyo ni nini? |
| Angela: | Hapana - lakini nimewahi kusikia kuhusu AIDS - Ukimwi… lakini… |
| Daktari: | Usijali, HIV ni virusi vinavyoambukia kupitia tendo la ndoa au damu, je umeshawahi kutiwa damu katika kipindi cha nusu mwaka uliopita? |

| | |
|---|---|
| Angela: | Hapana bado kabisaa. |
| Daktari: | Lakini umefanya mapenzi. Je umelala na wanaume wangapi? |
| Angela: | Eti wanaume wangapi? Daktari? |
| Daktari: | Au umelala na wengi ambao huwezi kujua idadi yao? Usiogope kunambia mimi ni daktari wako Angela. |
| Angela: | Daktari nilikuwa bado ni bikra, nilifanya mara moja tu na kijana mmoja basi. |
| Daktari: | Na kwa hivyo hakutumia kinga yaani mpira wa Kondom - kwa sababu angetumia mpira hungepata mimba, lakini unajua kwamba mara moja inatosha wewe kuambukizwa virusi vya HIV? Je ulimuuliza ikiwa yeye ana virusi au la? |
| Angela: | (Anashutuka) haiwezekani bila shaka hana virusi daktari. |
| Daktari: | (Kwa mzaha) Bila shaka haiwezi kuwa hivyo! Basi ngoja tukutoe damu tuifanyie uchunguzi, tia saini hapa. |
| SFX: | Sauti za karatasi, daktari akifungua kishubaka na kutoa sirinji. |
| Angela: | Ouchhh… |
| SFX: | Sauti ya Sirinji ya chuma ikiwekwa ndani ya kibakuli cha chuma. |
| Daktari: | Naam Angela, nina wagonjwa wengine kumi zaidi ambao wananisubiri. Wanahitaji kuhudumiwa katika muda wa dakika 10 zijazo. Kwa hivyo chukua makaratasi haya kayasome, njoo tena hapa wiki ijayo, uchukue majibu yako. Tumeelewana. |
| SFX: | Malango unafunguliwa. |
| Daktari: | Mwengine… |

**Sura ya pili: kwenye lango la shule.**

| | |
|---|---|
| SFX: | Wanafunzi wakitoka shule, sauti za magari na mabasi zinasikika. |
| Tom: | Sasa Djamila, huruhusiwi kutoka au vipi? |
| Djamila: | Hee unanifanya nijihisi kama mfungwa, mimi huenda out |
| Tom: | Lakini unajua tena katika dini yetu ya kiislamu msichana lazima asindikizwe na mtu mzima katika familia, kwa kawaida kakangu hunipeleka. Kwa hivyo nikikwambia Djamila tutoke siku moja ina maana hata kaka yako itabidi nimuombe idhini sio? Hmmmm, huo sio mpango poa! |

| | |
|---|---|
| Djamila: | Unajua sisi tunaamini bikra sana enhe hilo unalifahamu, hakuna kufanya mapenzi kabla ya kuolewa. |
| Tom: | Ndio hata sisi ni hivyo hivyo lakini wafikiri nani anayefuata mambo hayo siku hizi? |
| Djamila: | Sisi tunayafuata, mimi naamini ni salama zaidi kwa msichana kujiepusha na kufanya zinaa, kwa sababu mtu hutokuwa na wasiwasi juu ya lolote iwe ni mimba au mambo mwengine, kama jinsi wasichana wengine wanavyoingiwa na wasiwasi katika darasa letu… ah ngoja nikimbilie basi letu lile.… |
| SFX: | Basi linakaribia |
| Tom: | Wewe ni swahiba yake sana Annie. Kwa nini mnatofautiana hivyo, yeye kila mara yuko kwenye mambo ya simu, nguo yaani kwa ufupi yeye ni binti wa anasa tu. |
| Djamila: | Annie anafurahisha kweli, ni maskini kweli. Lakini nafikiri anapenda sana kupewa zawadi zawadi na raha nyinginezo kutoka kwa wanaume (anazungumza kwa aibu) namaanisha vitu ambayvo amekuwa akipokea. |
| Tom: | Djamila unanishangaza kweli yaani vitu vyote hivi anapokea kutoka kwa wanaume? |
| Djamila: | Sikiliza Tom, kwa nini humuulizi mwenyewe? Ikiwa unataka kujua mengi wewe mfuate ukamuulize mwenyewe. |
| Tom: | Je, ana rafiki wa kiume? Yaani mpenzi? |
| Djamila: | Kwa hakika, sitaki kuzungumzia suala hilo tafadhali… |
| Tom: | Je yule bwana namaanisha yule bwana mtu mzima hivi mwenye gari la kifahari ambaye huwa anamleta shule mara yningine? |
| Djamila: | (akicheka) yaani wewe umekuwa hakimu wa umri? Sio mzee vile unavyofikiria. |
| Tom: | Aha kwa hivyo unamfahamu sio? Hebu nambie unakuaje. |
| Djamila: | Sikiliza Tom, usifikiri unaweza kunitoa maneno kirahisi namna hiyo. Siendelei mbele na mjadala huo, tafadhali. Nimefikia kikomo, nenda ukamuulize mwenyewe. Kwa heri. |

**Sura ya tatu: Nyumbani, Annie anataka kutoka.**

| | |
|---|---|
| SFX | Sauti ya televisheni, vyombo vikiondolewa mezani. |
| Annie: | Mama nimeshaondoa kila kitu mezani sasa naenda kuwasabahi mashoga zangu. |

| | |
|---|---|
| Ma Tilly: | (Kando ya mic) Hmmmmmm. Haya Annie, lakini kumbuka kurudi mapema, saa mbili uwe umesharudi nyumbani, sawa… |
| SFX: | Mlango ukifunguliwa jioni… |
| Jet: | (Kando ya Mic) Pssssst, Annie. Niko hapa, njoo! |
| Annie: | (akifurahi) Jet! (wapigana mabusu) |
| Jet: | (Akitoa sauti ya kutulia ya mapenzi) sasa nambie twende kwangu au kwako? |
| Annie: | (Akicheka cheka) wewe mjinga kweli! Unajua lazima nirudi nyumbani kufikia saa mbili. |
| Jet: | Ahhhhh mpenzi hilo tu usitie shaka unajua usemalo ndo nitendalo ama vipi! |
| SFX: | Muziki wa kumalizia. |

**Sura ya nne: Sebuleni, jioni.**

| | |
|---|---|
| Anita: | Naam sasa, kwa vile tushajua mbivu na mbichi kwamba una ujauzito: je huyo alokutwika mzigo huo ni nani? Familia yake lazima iambiwe. |
| Angela: | Lakini nilikutana nae usiku mmoja tu. Hata simjui… |
| Anita: | Kwa hiyo ulilala nae na kupoteza ubikra wako kwa mtu usiyemjua hata jina? |
| Angela: | Jina lake anaitwa Pinto - ni jina la utani ni jirani yake mjomba. Lalya na Mo pia waliakwa, wanamfahamu vizuri. |
| Anita: | Aha kwa hiyo binamu zako walikusoza kwenye janga hili sio? Haya sasa basi nataka umpigie simu huyo Pinto. Umwambie mwenyewe kwamba una mimba yake… Haya shika simu… haraka mpigie… sasa hivi. |
| Angela: | Sina nambari yake mama… |
| Anita: | Sawa. Ngoja nimpigie ndugu yangu… kama wewe huna hiyo namba, subiri… |
| SFX: | Sauti ya simu inapigwa. |
| Angela: | (Kwa jazba) La, mama, tafadhali usifanye hivyo mama. |
| Billy: | (kwenye simu) Hallo |
| Anita: | Billy hujui ni kwa kiasi gani mapuuza yako yamesababisha balaa. |
| Billy: | Samahani? Eti nini? Mapuuza gani tena... wazungumzia kuhusu nini? |
| Anita: | (Akimkatiza) Mwambie huyo jirani yako… kijana aneitwa Pinto, awasiliane na mimi kwa nambari hiyo sasa hivi! Angela atakuja kuishi huko kwake, mwambie hivyo umesikia. |

SFX: Akata simu kwa hasira. Angela bado anaendelea kulia.

**Hitimisho**

Malaika wa kila mtu ni mchezo wa kuigiza uliotungwa na Romie Singh na kuhaririwa na Saumu Mwasimba. Na kufikia hapo ndio tumefikia mwisho wa kipindi cha sikiliza ujifunze kwa leo.

Jiunge nasi tena wiki ijayo wakati Angela atakapokumbuka usiku ule alokuwa katika sherehe na kujiuliza maswali mengi ambayo hayana majibu.

Kumbuka unaweza kusikiliza tena mchezo huu au kuwaambia marafiki wasikilize kupitia tovuti yetu kwenye mtandao wa Internet anuani yetu ni www.dw-world.de/lbe